

Mwongozo wa Kozi. Ufafanuzi wa Kibiblia

Alitupatia Maandiko: Misingi ya Ufafanuzi

MAELEKEZO YA KOZI

Wakristo wa Kiinjilisti hudhibitisha kuwa Maandiko ni Neno la Mungu lisilo na makosa. Lakini bado Wakristo wote hatukubaliani juu ya maana ya Mistari fulani au kifungu cha Maandiko, na tofauti hizi huathiri mafundisho na utendaji wa Wakristo. Sababu mojawapo ya kutokukubaliana ni kwamba kuna njia nyingi tofauti za kufanya tafsiri ya Biblia. Lakini tunajua njia sahihi inayofaa zaidi katika kutafsiri. Kozi hii itasaidia kujibu swali hilo. Huu ni Mfululizo wa masomo yanayohusu mada ya Alitupatia Maandiko: Misingi ya Ufafanuzi iliyotayarishwa na Huduma ya Third Millennium na kusimamiwa na Dr. Richard L. Pratt, Jr., pamoja na Maprofesa mabilmbali.

Malengo na Malengo Mahususi

Malengo

Katika Kozi hii, tumelenga kukamilisha yafuatayo:

1. Kuwa utaelewa kanuni za msingi za ufafanuzi wa Biblia, ikijumuisha istilahi na historia ya kihemeneutiki, mtazamo wa kibiblia kwa maana ya asili ya kipekee ya Maandiko na njia sahihi ya kubaini maana ya asili ya kifungu na kukitumia, kwa mkutadha wetu wa kisasa.
2. Utakuwa na hamu ya kusoma Maandiko kwa uangalifu na kugundua mbinu bora ya kuyatafsiri.
3. Kuwa utatumia miongozo ya kozi hii ili kukuza tabia zinazofaa katika utafsiri wa Biblia.

Malengo Mahususi

Ukitimiza yafuatayo, itaonyesha kuwa malengo mahususi yamefikiwa:

1. Pata alama za kuridhisha katika maswali na majaribio, kuonyesha kwamba unaweza kutambua kanuni za kimsingi za Tafsiri za Biblia, ikijumuisha istilahi na taarifa Muhimu za kuhusu historia ya Kihemeneutiki, vipengele muhimu vya kupitia ili kufikia maana, sifa ya kipekee za Maandiko, na kanuni kuu za kugundua maana ya asilia ya kifungu na kuweza kukitumia katika Mukutadha wetu wa kisasa.
2. Jibu maswali ya matumizi ya miongozo ya masomo, na kujizoeza kutumia mafundisho ya masomo kwa kifungu husika cha Biblia.

3. Shiriki kwenye Majadiliano ya kila wiki ambayo yanahusika katika kukagua masomo kupitia video za Thirdmill, ili kuelewa kwa ukamilifu jinsi ya kuzitumia katika maisha na huduma yako.

Orodha ya Moduli za Tafsiri za Biblia

1. Utangulizi wa Hermeneutiki za Kibiblia
2. Maandalizi Kwaajili ya Kutafsiri
3. Kuchunguza Maandiko
4. Mbinu za Kufikia Maana
5. Utata wa Maana
6. Kugundua Maana
7. Kutumia Maandiko
8. Matumizi ya Kisasa na Nyakati za Agano La Kale
9. Matumizi ya Kisasa na Agano Jipya
10. Utamaduni wa Biblia na Matumizi yake Sasa
11. Matumizi ya Sasa kwa mtu Binafsi

UFAFANUZI WA VIPENGELE VYA KOZI

Beji

1. Kila wiki ya Majadiliano katika kundi, tenga muda kwa ajili ya kufanya kazi pamoja na hati ya beji. Mwongozo huu wa kurasa mbili utatoa mwelekeo wa jumla kwa mkufunzi wako unapotafuta kukuza ujuzi huu muhimu wa huduma.
2. Katika wiki chache, sehemu ya muda wako wa majadiliano itatumika kupitia Mada za majadiliano zilizotolewa katika maagizo ya beji.
3. Ukisha kuwa na msingi mzuri wa majadiliano ya kikundi tumia wiki zilizobaki kufanya kazi ya Beji ya ***Wito kwa vitendo***.
4. Utatunukiwa beji endapo Mkufunzi wako atakaporidhika kuwa umekamilisha hatua, kwa kuzingatia maelekezo ya hatua za vitendo za Beji.

Moduli

1. Soma masomo, Tazama **video**, sikiliza **sauti**, au Soma **nukuu za somo**.
2. Kamilisha **Miongozo ya Somo** kwa kila Moduli. Tumia Miongozo ya masomo kujitayarisha kwa ajili ya ***maswali ya mtandaoni***.
3. Fanya majaribio kwa njia ya mtandao kwa kila moduli. Unaweza kufanya Majaribio mara nyingi kwa kadri uwezavyo, lakini itakupasa kusubiri saa moja kabla ya kurudia jaribio hilo. Alama za juu utakazopata katika jaribio zitatumika rasmi. Tunashauri upate angalau 80% kabla ya kushiriki katika majadiliano ya kila wiki ili kuhakikisha kuwa unaelewa dhana kwa usahihi.
4. Shirikiana na kundi lako katika *majadiliano* ya kila wiki, pamoja na mkufunzi wako, kwa kutumia ***Mwongozo wa majadiliano***. Majadiliano ni muhimu kwaajili ya kukuza ufahamu wako wa matumizi ya nyenzo za kozi, lakini pia yanakuza uwezo wako wa

kutumia dhana kwa usahihi katika maisha na huduma yako. Tunapoendelea mjadala wa kila moduli udumu angalau saa moja.

Mtihani wa Mwisho

Unaweza kufanya mitihani mara nyingi kama uwezavyo, lakini ni lazima usubiri saa moja kwa kila mtihani. Daraja lenye alama za juu, ndilo litachukuliwa kuwa rasmi, ni lazima ufikie 80% kwenye mtihani wa mwisho.

MADARAJA

Daraja la Mtihani wa mwisho linahesabiwa kama ifuatavyo:

1. Maswali ya majaribio yana thamani ya alama 30.
2. Mtihani wa mwisho una thamani ya 100.
3. Beji haitaathiri daraja lako, lakini lazima ikamilishwe kwa kuridhiwa na mkufunzi na iwekwe kwenye alama kuwa imekamilika katika orodha ya uhakiki wa mafunzo ya Biblia.

Ufaulu wa juu ni kuanzia 80%

Orodha ya Waliochangia kuandaa Kozi hii:

Dkt. Jimmy Agan ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya na Mkurugenzi wa Homiletics katika Seminari inayoitwa Covenant Theological Seminary.

Dkt. David R. Bauer ni mkuu wa shule ya Utafsiri wa Biblia na Profesa wa Kujifunza Biblia kwa kufuata Neno katika Seminari ya Theolojia ya Asbury.

Dkt. Bruce Baugus ni Profesa mshiriki wa Falsafa na Theolojia katika Seminari inayoitwa Seminari ya Theolojia Iliyorekebisha.

Dkt. Steve Blakemore ni Profesa wa Falsafa katika chuo Biblia kiitwacho Wesley Biblical Seminary.

Dkt. Darrell L. Bock ni Mkurugenzi mtendaji wa Ushirikiano wa Kitamaduni na Profesa mkuu wa utafiti wa masomo ya Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia ya Dallas.

Dkt. Stephen J. Bramer ni Profesa na Mwenyekiti wa Idara ya Ufafanuzi wa Biblia katika Seminari ya Theolojia ya Dallas.

Dkt. P.J. Buys ni Mkurugenzi Mshiriki wa Kimataifa wa Ushirika wa Theolojia iliyobadilishwa Dunia, na pia ni Profesa Msaidizi wa Utafiti wa Misiolojia katika Chuo Kikuu cha Northwest Potchefstroom, huko Afrika Kusini.

Dkt. David W. Chapman ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya na Akiolojia katika Seminari ya Theolojia ya Agano.

Dkt. Gary Cockerill ni Profesa wa Agano Jipya na Theolojia ya Biblia katika Seminari ya Wesley.

Dkt. Brandon D. Crowe ni Profesa Msaidizi wa Agano Jipya Katika Seminari ya Theolojia katika chuo cha Westminster Seminari.

Dkt. Andrew Davis ni Mchungaji kiongozi katika Kanisa la First Baptist Church ya Durham, NC, na Profesa Mwalikwa wa Historia ya Theolojia katika Seminari ya Southeastern Baptist Theological.

Dkt. Howard Eyrych ni Mkurugenzi Mshauri wa Maswala ya Biblia katika Seminari ya Kitheolojia ya Birmingham Mchungaji Mshauri katika huduma ya Kanisa la Briarwood Presbyterian.

Dkt. Matt Friedeman ni Profesa wa Uinjilisti na Uanafunzi katika Seminari ya Wesley.

Mch. Michael J. Glodo ni Profesa Mshiriki wa Masomo ya Biblia katika chuo cha Reformed Theological Seminary katika Kampasi ya Orlando, Florida.

Mch. Thad James, Jr. Ni Makamu wa Raisi katika Idara ya Taaluma katika Seminari ya Theolojia inayoitwa Birmingham.

Dkt. Dennis E. Johnson Ni Mtaaluma mkuu na Profesa wa Theolojia kwa Vitendo katika seminari ya Westminster Seminary California.

Dkt. Craig S. Keener Ni Mkuu wa kitivo cha Masomo ya Kibiblia katika seminari ya Asbury Theological Seminary.

Dkt. Ghassan Khalaf ni Profesa wa Idara ya Masomo ya Biblia katika Seminari ya Arab Baptist huko Mansourieh El Maten, Lebanon.

Dkt. Daniel L. Kim ni Profesa mshiriki wa Agano la Kale katika seminari ya Covenant Theological.

Dkt. Michael J. Kruger ni Raisi na Profesa wa Agano Jipya katika Semina ya Theolojia ya Reformed huko Charlotte, N.C.

Dkt. David T. Lamb ni Profesa Mshiriki wa Agano la Kale katika Seminari ya Theolojia ya Biblia.

Dkt. Robert G. Lister ni Profesa mshiriki wa Masomo ya Biblia na Theolojia katika Shule ya Theolojia ya Talbot.

Dkt. Robert K. MacEwen ni Mkurugenzi wa Idara ya Theolojia katika Shule ya Theolojia ya Asia Mashariki.

Dkt. Miguel Nunez ni Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kimataifa la Baptist katika Jamhuri ya Santo Domingo, Dominican.

Dkt. Luis Orteza ni Profesa Msaidizi Mshauri katika Seminari ya Theolojia Birmingham.

Dkt. John Oswalt Ni Profesa wa Agano la Kale katika Seminari ya Kitheolojia ya Asbury.

Mch. Youssef Ourahmane Alishiriki katika kutoa Mafunzo kwa viongozi wa Kanisa katika shule inayoitwa Timotheo nchini Algeria.

Dkt. Jonathan T. Pennington ni Profesa Mshiriki wa Tafsiri za Agano Jipya na Mkurugenzi wa Utafiti wa Masomo ya uzamivu katika seminari ya The Southern Baptist Theological Seminary.

Dkt. Greg Perry ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya na Mkurugenzi wa Mpango wa huduma za Mjini katika Seminari ya Covenant Theological.

Dkt. Robert L. Plummer ni Profesa Mshiriki wa Tafsiri za Agano Jipya katika Seminari ya Southern Baptist Theological.

Dkt. Vern S. Poythress ni Profesa wa Tafsiri ya Agano Jipya katika Seminari ya Westminster Theolojia Seminari na Mhariri wa Makala ya Kitheolojia itwayo Westminster Theological Journal.

Dkt. Scott Redd ni Profesa Mshiriki wa Agano la Kale na Mkuu wa seminari ya Theological Kampasi ya Washington D.C.

Dkt. Philip Ryken ni Raisi wa Chuo cha Wheaton.

Dkt. Glen G. Scorgie ni Profesa wa Theolojia katika Seminari katika Seminari ya Bethel huko San Diego.

Dkt. James D. Smith III ni Profesa Mshiriki wa Historia ya Kanisa katika Seminari ya San Diego, na Profesa wa Dini katika chuo kikuu cha San Diego.

Dkt. K. Erik Thoennes ni Profesa wa Biblia na Masomo ya Theolojia, katika chuo kikuu cha Biola Talbot shule ya Theolojia, na Mwenyekiti wa kitivo cha Biblia na Masomo ya Theolojia.

Mch. Dkt. Stephen Tong ni Mwinjilisti na Mwanatheolojia Mashuhuri wa China, Mhamasishaji wa Injili iliyorekebisha, na Mwanzilishi wa Huduma ya Kimataifa ya kiinjilisti inayoitwa Stephen Tong (STEMI) na mwinjilisti wa Kanisa la Reformed na Seminari ya Indonesia.

Dkt. Stephen Um ni Mchungaji Kiongozi wa Kanisa linaloitwa Citylife Presbyterian Church huko Boston.

Dkt. Miles Van Pelt ni Profesa wa Agano la Kale na Mtaaluma mkuu katika Seminari inayoitwa Reformed Theological Seminary.

Dkt. Simon Vibert ni Mchungaji kiongozi wa Kanisa linaloitwa Kanisa la Kristo huko Virginia Water, England, na alikuwa Makam mkuu na Mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri huko Wycliffe Hall, Oxford.

Dkt. Brian J. Vickers ni Profesa mshiriki wa Tafsiri za Agano Jipya katika Seminari inayoitwa Southern Baptist Theological Seminary na Mhariri Masaidizi katika Makala ya Kitheolojia inayoitwa Southern Baptist Journal.

Dkt. Carey Vinzant ni Profesa msaidizi wa Theolojia ya Utaratibu katika seminari ya Wesley Biblical Seminary.

Dkt. Peter Walker ni Profesa wa Masomo ya Biblia katika shule ya huduma iitwayo utatu.

Dkt. Daniel B. Wallace ni Profesa wa Masomo ya Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia ya Dallas.

Dkt. Guy Waters ni Profesa wa Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia iliyorekebishwa.

Dkt. Stephen J. Wellum ni Profesa wa Theolojia ya Kikristo katika Seminari ya kitheolojia inayoitwa Southern Baptist.

Dkt. Donald S. Whitney ni Profesa wa maswala ya Biblia na Kiroho, pia ni Makamu mshiriki wa Shule ya Theolojia katika Seminari inayoitwa Southern Baptist Theological Seminary.

Dr. Sanders L. Willson ni Mhudumu kiongozi katika Kanisa la Second Presbyterian huko in Memphis, TN, Pia ni Mhudumu katika Bodi ya Gospel Coalition, katika chuo kikuu kiitwacho Union University na katika Seminari ya Reformed.